



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
HALMASHAURI YA CHAMWINO  
JIMBO LA CHAMWINO NA MVUMI**

Kumb. Na. HWC/CE.3/I VOL.I/A

20 Septemba, 2020

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA**

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la CHAMWINO na MVUMI kwa kuzingatia kanuni ya 14 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na kanuni ya 12 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenyе sifa na uwezo wa kujaza nafasi za Watendaji wa Uchaguzi Mkuu utakaofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 kama ifuatavyo:-

1. **MSIMAMIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA (NAFASI. 892).**
2. **MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA (NAFASI. 1784).**
3. **KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA (NAFASI. 892).**
  - A. **SIFA ZA WAOMBALI WA NAFASI YA MSIMAMIZI AU  
MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA**
    - (a) Awe Raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
    - (b) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa;
    - (c) Awe mwadilifu, mtii fu na mwenye akili timamu;
    - (d) Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri. Pia, anayeweza kuyaelewa Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na
    - (e) Ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo anaomba.
  - B. **SIFA ZA WAOMBALI WA NAFASI ZA KARANI MWONGOZAJI WA  
WAPIGA KURA**
    - (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
    - (b) Awe mkazi wa kata ambayo atafanya kazi ya kuongoza wapiga kura;
    - (c) Ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo anachofanya kazi;
    - (d) Awe mwadilifu, mtii fu na mwenye akili timamu;
    - (e) Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuyaelewa Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na
    - (f) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.

### C. MALIPO

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo:-



- i. Msimamizi wa Kituo siku ya Uchaguzi atalipwa posho ya Tzs. 35,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs 15,000 kwa siku moja na nauli Tzs 20,000;
- ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Tzs. 30,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs 15,000 na nauli Tzs 20,000; na
- iii. Karani Mwongozaji Wapiga Kura atalipwa posho ya Tzs 30,000 kwa siku moja na posho ya chakula Tzs 15,000.

### D. MASHARITI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE

- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.
- Maombi yote yaambatane na Vyeti vya taaluma, nakala za Vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita au kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa kwa mujibu wa Tangazo hili.
- Waombaji waambatishe picha mbili 'Passport size' za hivi karibuni.
- Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
- Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 27 Septemba , 2020.**

Anuani ya kutuma maombi ya kazi ni:-

Msimamizi wa Uchaguzi,  
Jimbo la Chamwino na Mvumi,  
S. L. P . 1126,  
**CHAMWINO - DODOMA.**  
Email.ded@chamwinodc.go.tz  
Tovuti:[www.chamwinodc.go.tz](http://www.chamwinodc.go.tz)



**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
JIMBO LA CHAMWINO NA MVUMI.**